# OFIASI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
# SHULE YA SEKONDARI GONGWE, S.L.P 56, KILOSA.

## MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GONGWE WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021.

KUMB NA. GSS/FI/SEC/ …………………………………………………
JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………
NAMBA YA MTIHANI ……………………………………………………
SHULE ATOKAYO …………………………………………………………

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule hii mwaka ……………………
Shule ya Sekondari Gongwe ni Shule ya mchanganyiko na ya kutwa (day school) ipo umbali wa Km 39 kaskazini mwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Tarafa ya Magole, Kata ya Mvumi.
Unapaswa kuripoti shuleni mwanzoni mwa muhula wa kwanza wa masomo utakao anza rasmi tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti shuleni 31/01/2021 (ndani ya siku 21 ), ukishindwa kuripoti bila taarifa hutopokelewa mpaka upitie kwa Mratibu elimu kata ya Mvumi.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

a) Sare ya shuleni :-

**Wavulana** – Shati 2 nyeupe mikono mifupi

- Suruali 2 kijani kibichi mshono **wenye marinda mawili na upindo kwa chini** wa heshima
- Soksi nyeupe zenye urefu wa kawaida josi 2
- Sweta rangi ya kijani kibichi.
- Viatu vyeusi vya kamba visiwe na visigino virefu jozi 2
- Tshirti moja ya kuvaa darasani

**Wasichana** - shati 2 nyeupe mikono mifupi

- Sketi 2 kijani kibichi mshono wa **rinda box mbele na nyuma na ndefu**
- Viatu vyeusi vilivyo na kisigino kirefu vyevye kamba jozi 2
- Soksi nyeupe ndefu jozi 2
- Tishirti 1 ya kuvaa darasani

b) Kwa Waislamu wa kike **wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeupe isiyo na mapambo inayofunika mikono yote na miguu hadi magotini** mradi wanyoe nywele zote za kichwani.

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni:-
**Wavulana** – Tracksuit rangi nyekundu jozi 1. Raba za michezo jozi 1.
**Wasichana** – Tracksuit rangi nyekundu jozi 1, raba za michezo jozi 1

**NB:** - Sare zote zishonwe kwa kufuata maelekezo kutoka uongozi wa shule vinginevyo zenye dosari hazitaruhusiwa shuleni **'HASA MODO na SKETI FUPI'**

- **Tshirt za kuvaa darasani zitapatikana shuleni**.

2.2 Daftari 15 counter book, kalamu za wino wa blue au nyeusi 10 penseli 2, mkebe wa hesabu 1, jalada la kutunzia kumbukumbu 1 (file)

- Kamusi ya kingereza(dictionary) na kamusi ya Kiswahili kwa atakaye ona umuhimu wa kuwa nayo

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Uwapo shuleni unapaswa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo, na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima .
c. Kushiriki kikamilifu ratiba zote za masomo darasani ikiwa ni pamoja na kuandika nukuu za masomo yote majaribio pamoja na kufanya mitihani ya mihula yote pamoja na mitihani ya nje.
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i. Kutunza mali za umma.

## 3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa masomo

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi , kubeli na kadharika.
e. Kupigana au kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya uma
g. Kudharau bendera na wimbo wa Taifa
h. Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba
i. Kuoa au kuolewa
j. Kuongoza au kushiriki vurugu, uvunjifu wa amani na usalama wa shule au watu.
k. Kukataa adhabu kwa makusudi
l. Kuwa na simu ya mkononi.
m. Kuto kuhudhuria vipindi vya darasani na kuto kuandika nukuu za masomo

Tunakutakia maandalizi mema Karibu Gongwe Sekondari.

……………………………

NURU H. PANGISA
MKUU WA SHULE

MAWASILIANO:- 0787 – 166 – 531 /0754 – 424 – 725 (MKUU WA SHULE)
0654 – 891 – 210 / 0683 – 215 – 831 (MAKAMU MKUU WA SHULE )

**PRESIDENT'S OFFICE -RALG**
**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

**Gongwe secondary school**
**P.0 Box 56**
**Kilosa**
**.................................**

Please Examine The Student (Name)....................................................................................... To his/her fitness to undego training studying and subsequently work.

# MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the student named above and consider his/her fitness for re-engagement as above. This is certified by the following result of may examination:

1. Bilhazias .......................................
   ..................................................
2. Jaundice ......................................
   ......................................................
3. Scabies ........................................
   ......................................
4. Typhoid ........................................
   .........................................................................
5. Tropical ulcer ............................
6. Abscesses ...................................
7. Asthma........................................
8. Leprosy ........................................
9. Small pox ....................................
   ........................................................................
10. Heart failure ..............................
    ..................................................................
11. Cystitis ........................................
    ..............................................................
12. Diabetes......................................
    ..................................................
13. Epilepsy ......................................
    ...........................
14. STDs ...........................................
    not noted ...........
15. Headache ...................................
16. Skin diasease
17. Osteomylitis
18. Bronchopneumonia
19. TB

Other examinations

1. Eyes
2. Chest
3. Abdomen
4. Haemoglobin
5. Any abnormalities noted
6. Any chronic complaints

Note: in case of TB and Bilhazias it is recommended that a student should attend a clinical/medical treatment before he/she comes to school.

Name and signature of Medical officer/Examiner

............................................................................................................

Desination official stamp

..................................................................................................................................................................

**Date** .....................................